UMUHIMU WA ELIMU KUHUSU MAHAKAMA KAMA HATUA YA MSINGI KATIKA UTATUZI WA MIGOGORO KATIKA JAMII

MAADHIMISHO YA SIKU YA SHERIA TANZANIA

FREDERICK.WEREMA
2/2/2011

UMUHIMU WA ELIMU KUHUSU MAHAKAMA KAMA HATUA YA MSINGI YA UTATUZI WA MIGOGORO KATIKA JAMII

Mheshimiwa Dr Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Anne Makinda, (Mb) Spika wa Bunge la Tanzania

Mheshimiwa Mohamed Chande Othman, Jaji Mkuu wa Tanzania;

Mheshimiwa Jaji Mkuu Mstaafu Augustino Stephen Lawrence Ramadhani

Mheshimiwa Celina Ombeshi Kombani, (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria;

Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani;

Mheshimiwa Jaji Kiongozi;

Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu;

Waheshimiwa Mabalozi

Viongozi wa Serikali;

Wastahiki sana Viongozi wa Madhehebu mbalimbali

Mheshimiwa Msajili wa Mahakama ya Rufani; na Mahakama Kuu;

Waheshimiwa Mahakimu wa ngazi zote;

Rais wa Chama Cha Mawakili;

Wasomi wenzangu Mawakili;

Mabibi na Mabwana;

"...Serikali nitakayoiunda siku chache zijazo itakuwa na vipaumbele 13 vifuatavyo:

1. .....

2. ....

3. ....

10. kuimarisha utawala bora, demokrasia, utawala wa sheria, haki za binadamu na kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya rushwa, dawa za kulevya, matumizi mabaya ya madaraka na ubadhirifu wa mali ya umma. Kwa ajili hiyo tutaendelea kuvijenga na kuviwezesha kiraslimali, kimuundo na kisheria vyombovinavyoongoza mapambano hayo na vile vya kutoa na Kusimamia haki nchini." J.M. Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, katika Hotuba ya Uzinduzi rasmi wa Bunge la Kumi, 18 Novemba 2010"

Leo ni siku ya maadhimisho ya kuashiria kuanza kwa Mwaka Mpya wa Shughuli za Mahakama ya Tanzania. Kama kawaida na desturi siku hii huadhimishwa kwa hotuba za viongozi wa Mahakama; Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mawakili wa Serikali wafawidhi huko mikoani; Rais wa Chama cha Mawakili au wawakilishi wake huko mikoani.

Ni siku maalum ambapo Wakuu wote wa Mihimili ya dola inayotamkwa katika Masharti ya Ibara ya 4 ya Katiba ya Nchi wanashiriki pamoja kuizindua siku hii. Ni siku ambayo tunajumuika na Mkuu wa Dola; tunamwona Spika wa Bunge la Tanzania; na Jaji Mkuu tukikumbashana tulikotoka na tuendako. Ingawa mara zote Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Spika hawatoi

hotuba lakini kuwapo kwao katika shughuli hii ni ushahidi wa kutosha wa namna wanavyoenzi shughuli za mahakama za utoaji wa haki. Utaratibu huu ni mzuri sana kwa sababu hauingilii Uhuru wa Chombo chochote isipokuwa unaimarisha mahusiano ya Kikatiba ya Mihimili ya Dola ya Tanzania. Sisi Mawakili wa Serikali tunapenda utaratibu huu uimarishwe na kuendelezwa. Inafaa tufikirie kuifanya siku hii iwe maalum ya kutathmini juu ya utoaji wa haki nchini kwa Mwaka uliotangulia; siku ambayo tutajadili mambo maalum kwa kina. Tunaona njia hii itatusaidia kupata maoni ya wadau wetu kuliko ilivyo sasa.

Kama wote tunavyofahamu, tunaadhimisha siku hii kitambo kidogo tangu yalipofanyika mabadiliko ya kubadilisha kwa amani uongozi wa juu wa Mahakama kutokana na kustaafu kwa mujibu wa Sheria Jaji Mkuu

aliyemaliza kipindi chake punde. Kwa ajili hiyo, ninachukua nafasi hii na kwa niaba ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kumpongeza sana Mheshimiwa **Mohamed Chande Othman** kwa kuteuliwa kwake na Rais kuwa Jaji Mkuu wa Tanzania. Ofisi yangu na Mawakili wa Serikali wote tunakuahidi ushirikiano wetu wenye manufaa ya maana katika utendaji wa Kazi na kama ilivyo ada tunakuombea kwa Maulana, mwingi wa rehema, akujalie afya njema; akujalie busara na hekima; akupe ujasiri ili uweze kumudu kazi hii muhimu katika utoaji wa Haki. Watanzania watakuona wewe kama ni nuru ya Haki na wafanyakazi wenzako watakuona kama mkombozi wao katika taabu zinazotokana na kile kinachosemekana ni maslahi yao duni. Utakuwa kinga kwa majaji, ngao itakayokinga **uhuru wa Mahakimu** kuamua mashauri bila hofu; au kuingiliwa na hisia za

kijamii pale ambapo maamuzi ya Mahakimu hayawafurahishi baadhi ya watu. Utakuwa pia Kimbilio kwa wale wanaodhani haki zao zimeminywa kwani ni rahisi mlalamikaji kukuona wewe kuliko yeye kumwona Jaji au Hakimu aliyesikiliza au anayesikiliza shauri lake. Nami ninaona hilo ni jambo jema la kuendeleza.

Kwa aina ya pekee, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Jaji Mkuu Mstaafu **Augustino Stephen Lawrence Ramadhani** kwa kuiongoza Mahakama ya Tanzania kwa ustadi wa kutosha na kuifikisha Mahakama pahala pazuri. Katika Kipindi chake tuliona hatua thabiti na nia ya dhati ya kufanya mabadiliko na kuleta maboresho katika Mahakama ya Tanzania. Mimi na Mawakili wenzangu tunamtakia kila mzee huyu kheri katika maisha ya kustaafu lakini tunamwomba

aslani asiache kalamu yake maridhawa ili tuweze kufaidika na maandiko yake katika tasnia ya sheria.

Ninawapongeza sana Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani; Majaji wa Mahakama Kuu; Mahakimu; wafanyakazi wa Mahakama wa ngazi zote; Mawakili Binafsi na Mawakili wa Serikali kwa Kazi nzuri ya usimamiaji na uteteaji wa Haki Nchini mwetu kwa Kipindi kilichopita. Tukumbuke kwamba katika Mwaka wa jana maadhimisho haya yalibeba maudhui mahsusi yaliyojikita katika Kuangalia *"Mahakama ikiwa Mdau wa Maendeleo katika Taifa na Umuhimu wa Kuboresha Mazingira yake ya Kazi ili iweze kutoa Huduma bora zaidi"*. Ninadhani kwa hakika kwamba tathmini imefanywa kuhusu maboresho yaliyofanywa tangu tulipoachana katika maadhimisho ya Mwaka jana ili kufahamu uimara wetu kwa pamoja au mmoja mmoja;

na changamoto ambazo bado tunazo. Bila kufanya hivyo ni rahisi kupoteza mwelekeo na kuanza kutangatanga nyikani jambo lisiloleta tija katika shughuli za Utoaji wa Haki nchini. Ninashauri kwamba tutafute nafasi ya kufanya tathmini hiyo kama hatujaifanya bado. Kwa mfano ingekuwa ni bora kurejea kulikofikiwa wazo la kuanzishwa kwa **mfuko wa Mahakama** kama njia ya kuimarisha dhana ya Uhuru wa Mahakama kifedha; suala la ucheleweshaji wa mashauri likoje sasa; Bajeti tuliyopata ya ongezeko la asilimia 50 juu ya bajeti iliyotangulia ilisaidiaje kumaliza tatizo la mlundikano wa mashauri; hali ya kesi za mabenki limefikia wapi; je kuna nafuu? Suala la matumizi ya TEKNOHAMA lililofanikishwa na **Mfuko wa Investment Climate Facility for Africa** limetusaidia vipi katika kuboresha utoaji wa haki? Mambo ni mengi ila ni vema kufahamu kwamba kikombe cha raslimali siku

zote hakijai kikasheheni, isipokuwa **kinakupwa nusu** na siku zote kikombe kilichokupwa nusu kimejaa nusu pia yaani **a half empty cup is also half full.** Maana ya msemo huu ni kwamba tutumie kidogo tulichonacho kwa hayo tunayoyaweza, na yaonekane. Nimeona umuhimu wa kuvinjari kwa yaliyopita, ingawa waswahili wa Mrima waamba, **Yaliyopita si ndwele, tugange yajayo**. Inafaa Tuyafanye yaliyopita kuwa jiwe la kona kuyahimili yale yajayo, tukiyaganga kwa ustadi.

Maudhui yetu kwa Mwaka huu ni **UMUHIMU WA ELIMU KUHUSU MAHAKAMA KAMA HATUA YA MSINGI YA UTATUZI WA MIGOGORO KATIKA JAMII.** Suala la ufahamu kuhusu Chombo cha Mahakama; Mamlaka ya ngazi mbali mbali za Mahakama; Utaratibu au Kanuni zinazofuatwa na Chombo hiki katika kutekeleza shughuli zake za utoaji wa Haki ni muhimu sio tu kwa

Wadau wa Mahakama ila hata Majaji; Mahakimu; Mawakili; Makarani wa Mahakama na maafisa wengine wanaotekeleza amri za Mahakama au kukaza hukumu za Mahakama. Usemi wa Elimu haina Mwisho unapaswa kuwa ni mwongozo sahihi kwetu tunaohusika na Mamlaka ya Mahakama. Kwani kitakuwa kiama cha kweli kama tutadhani tunajua bila kujikumbusha na kutafiti kwanza na kila mara.

Mamlaka yenye Kauli ya Mwisho ya utoaji wa Haki nchini mwetu kwa Masharti yaliyomo kwenye **Ibara ya 107A** ya Katiba ni Mahakama. Katiba imeainisha kinagaubaga kitakachoiongoza Mahakama katika kutoa uamuzi wa mashauri ya madai na jinai kuwa ni Sheria na Kanuni mahsusi zinazotajwa katika **Ibara ya 107A(2)** kuwa ni:

a) Kutenda haki kwa wote bila kujali hali ya mtu kijamii au kiuchumi;

b) Kutochelewesha haki bila sababu ya Kimsingi;

c) Kutoa fidia ipasavyo kwa watu wanaoathirika kutokana na Makosa ya watu wengine; na kwa mujibu wa sheria mahsusi iliyotungwa na Bunge;

d) Kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro;

e) Kutenda haki bila kufungwa kupita kiasi na masharti ya kiufundi yanayoweza kukwamisha haki kutendeka.

Masharti yaliyomo Katika **Ibara ya 107B** yanahimiza jambo kubwa la kuzingatiwa katika utoaji wa Haki kwa maneno yafuatayo:

"Katika kutekeleza mamlaka ya utoaji haki, mahakama zote zitakuwa huru na zitalazimika kuzingatia tu masharti ya Katiba na yale ya sheria za nchi."

Mamlaka ya utoaji wa Haki yanatokana na ukweli kwamba ni lazima kuwe na njia ya kutatua migogoro katika jamii. Kama tulivyoona katika masharti hayo, Mamlaka ya Kutatua migogoro si Mahakama pekee. Kuna Mabaraza ya Kata; Baraza la Ushindani; Mabaraza ya Ardhi; Baraza la Usuluhishi; Baraza la Kodi; kinachoainishwa ni kwamba maamuzi yanayotolewa na vyombo hivyo hatimaye yaweza kufikishwa Mahakamani. Kwa maoni yangu umuhimu wa awali wa kutoa elimu unaweza kuwa katika maeneo yafuatayo:

a) Utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi. Watu wengi wanaingia katika migogoro kutokana na ukosefu wa mawasiliano na maridhiano. Kila mgogoro, isipokuwa ile inayohusiana na jinai, inaweza kumalizika ya usuluhishi. Migogoro ya mipaka ya ardhi au milki ya ardhi; mirathi; milki ya mali inayohamishika; ndoa; migogoro ya Kazi, biashara n.k. elimu hii inapaswa kutolewa kote nchini na kuhamasisha watu kupenda kuitumia kwa kuwa inaimarisha mahusiano ya watu zaidi kuliko utaratibu wa kesi mahakamani ambapo anayeshinda anachukua haki yote. Bahati mbaya sana tunahitaji kuwahamasisha baadhi ya Mawakili;

Mahakimu na hata majaji ambao wanaona utaratibu huu unapoteza muda; au kama ni kwa Mawakili unawanyima mapato ya biashara ya uwakili wanayoilipia kodi;

b) Jambo la pili ni elimu ya Muundo na Mamlaka ya Mahakama kutegemeana na viwango vya fedha na eneo. Mahakama zetu zinafuata vidato au ngazi;

c) Jambo la tatu ni matumizi ya washauri wa Mahakama na Matumizi ya Sheria za mila katika Mahakama za Mwanzo. Sheria inatambua ushirikishwaji wa wananchi katika utoaji wa haki. Kazi za washauri wale ni kuisadia Mahakama kufikia haki. Wazee wale wanapaswa

kushauri kuhusu mila ya eneo husika kwa jambo lililo mbele ya Mahakama. Kwa mfano, kama kuna uamuzi wa kulinganisha thamani ya ng'ombe na Mbuzi katika eneo lao, wanapaswa kusema ng'ombe mmoja ni mbuzi wangapi? Hiyo si kazi ya Hakimu. Mahakimu nao wanapaswa kujifunza juu ya mambo hayo badala ya kuamua shauri kwa njia ambayo inaleta manung'uniko;

d) Tunahitaji kutoa elimu juu ya nini cha kufanya pale ambapo Mahakama imetoa uamuzi ambao hauridhishi mdaawa. Ipo tabia ya wadaawa kutaka maamuzi ya Mahakama yatenguliwe kiutawala kwa kulalamika kwa Wakuu wa

Wilaya, Mikoa, Wabunge, Mawaziri, Waziri Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano. Hukumu ya Mahakama haitenguliwi kwa njia hizo isipokuwa kwa kukata rufaa kwa muda ulioainishwa;

Migogoro ni matokeo ya Mahusiano ya Kiuchumi na Kijamii. Inaweza pia kutokea kama sehemu ya siasa au utamaduni. Inachukua muda mwingi na raslimali kuishughulikia. Inaweza kufifisha mahusiano katika jamii na kuhatarisha umoja na amani. Migogoro inaweza kudunisha maendeleo katika jamii. Tunahitaji ubunifu katika kutatua migogoro katika jamii kwa lengo la kupunguza kesi mahakamani. Tunahitaji pia kupunguza malalamiko yanayoharibu taswira ya Mahakama na yanayotokana na watu kutoelewa mamlaka au muundo wa Mahakama; au ufahamu wa

Sheria. Aidha, tunapaswa kuchangia katika kuhamasisha watu kuheshimu utawala wa kisheria. Ni Maoni yangu kwamba **rai ya kutoa elimu kuhusu Mahakama kama hatua ya Msingi ya Utatuzi wa Migogoro Katika jamii** inatolewa kwa wakati ulio mwafaka, wakati ambao, kwa bahati mbaya kuna dalili za watu kujichukulia Sheria Mikononi bila kujali uwepo wa Mamlaka ya Mahakama kama Chombo chenye kauli ya mwisho katika kutoa haki.

Maslahi ya Taifa letu, vyombo vyake na Watu wake yatalindwa na **Utawala wa Sheria** na mfumo wa watu wanaoheshimu sheria. Elimu hii inayotegemewa itatusaidia kulifikia lengo hili la Kikatiba la ushirikishwaji. Ingawa **Kikombe chetu cha raslimali tunakifahamu** jambo hili linahitaji raslimali lukuki. Ni eneo muhimu la ushirikiano baina ya Mahakama na Taasisi za Kiraia au

Asasi zisizokuwa za Serikali. Changamoto kubwa ni kuwa wengi wa hawa hawaendi pasipo rupia. Wengine ni hodari wa kuchangia sherehe za harusi, kitchen Party, na maafali kuliko meeneo haya.

Nimalizie kwa kuwatakia kila la kheri katika Mwaka huu wa Kazi. **Inawezekana, timiza wajibu wako. Ninawashukuru sana kwa kunisikiliza.**

Mungu Ibariki Afrika,

Mungu Ibariki Tanzania